OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU

SIMU: 0738111133/0719711512

SHULE YA SEKONDARI RUSESA
S.L.P 354
KASULU
10/12/2020

KUMB NA: RSS/S3694/JI/FI/16/12

Mwanafunzi.....

S/Msingi/Kijiji.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA RUSESA KIDATO CHA KWANZA 2021

Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Rusesa kwa mwaka 2021. Mhula wa masomo unaanza tarehe 11-01-2021.

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11-01-2021 hadi 30-01-2021.

Shule ya sekondari Rusesa ni ya wananchi, ya kutwa mchanganyiko. Ipo umbali wa meta 250 kutoka barabara ya Kasulu - Kigoma na kilometa 57 kutoka Makao makuu ya Wilaya ya Kasulu. Shule inafundisha masomo yote kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili.

MAMBO MUHIMU YATAKAYOGHARIMIWA NA MZAZI

1.1 SARE ZA SHULE

WAVULANA	WASICHNA
a. Suruali mbili (2) rangi ya damu ya mzee kitambaa cha Istem zenye mifuko miwili(2) na mmoja nyuma usio wa kubandikwa wala zipu (pisto au modo za suruli haziruhusiwi) b. Shati mbili (2) nyeupe za tetroni mikono mifupi na singland nyeupe inayovaliwa ndani ya shati. c. Viatu jozi mbili (2) vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba. d. Soksi jozi mbili (2) nyeusi e. Mkanda mweusi wa ngozi f. T-shit ya bluu na sweta ya rangi ya bluu	a. Sketi mbili (2) za rangi ya damu ya mzee kitambaa cha Istem. Zenye urefu wa kugusana na soksi na ziwe na rinda box tano(5) b. Shati mbili (2) nyeupe za tetroni mikono mifupi Shumizi nyeupe inayovaliwa ndani ya shati na skin tight. Kwa waislam washone nusu kanzu. Hijabu ifanane na shati la shule. c. Viatu jozi mbili (2) vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba. d. Soksi jozi mbili (2) nyeupe e. T.shit ya bluu naswetaya rangiya bluu

1.2. VIFAA VYA KITAALUMA

a/ Daftari tisa (9) kubwa (counter book quire 2/3) na ndogo (13) kumi na tatu za English Orientation na mazoezi.

b./Kamusi ndogo ya kiingereza (English- English Dictionary)
c/ Mkebe, Rula, na Kalamu za kutosha. d/ File binafsi la kutunzia mitihani na kumbukumbu zingine.

e/ Kila mwanafunzi awe na ream yake mwenyewe atakayoitumia wakati wa mitihani na mazoezi mengine.

1.3. VIFAA VYA MICHEZO

WASICHANA	WAVULANA
i. Track suit rangi ya bluu ii. Viatu vya michezo maarufu kama raba iii. Sketi ya kijani	i. Bukta na track suit ya bluu (jezi ya Chelsea) ii. Viatu vya michezo (njumu) iii. Soksi ndefu za kandanda (stockings)

SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 iliyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Shule inazingatia pia miongozo inayotolewa na Wizara zenye dhamana ya Elimu nchini zenye jukumu la uendeshaji na usimamizi wa elimu. Mwanafunzi anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo ndani na nje ya mazingiri ya shule; i/ Heshima kwa watu wote bila kujali cheo, umri, rangi, dini au chama.

ii/ Kila mwnafunzi anatakiwa kujali na kathamini mda kwa kuwahi mara moja wanapohitajiwa, kukaa kimya darasani, kuhudhuria masomo bila kukosa na kuhudhuria mikutano kama Mabaraza ya shule.

iii/ Kila mwanafunzi awapo shuleni ni lazima ashiriki kikamilifu katika shughuli zote za masomo, uzalishaji mali, usafi wa mazingira na michezo. iv/ Sharti mwanafunzi afahamu vyema nipaka ya shule.

v/ Mwanafunzi ahakikishe anatunza usafi binafsi wa mwili wake na mazingira ya shule.

Vi/ Nywele ndefu ,kusuka na kufuga ndevu ni marufuku.
Vii/ Lugha ya mawasiliano ni kiingeleza tu uwapo shuleni.

Viii/ Huruhusiwi kuongea kilugha uwapo mazingira ya shule, darasani au nje ya darasa.

X/ Hauruhusiwi kuwa nje ya darasa muda wa msomo bila ya kengele au tangazo kutoka kwa mwalimu.

Xi/ Unalazimika kuwa mwanachama wa vikundi mbalimbali vilivyopo shuleni vya kuhamasisha afya, utunzaji wa mazingira, uelimishaji rika, ukakamavu (scout) na vilabu vya masomo.

MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI

i/Wizi. ii/Uasherati na ushoga. iii/Ubakaji na ukabaji. iv/ Kupiga au kupigana v/Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya vi/ Kuoa , kuolewa au kutoa mimba. vii/ Kuharibu kwa makusudi mali ya umma. Viii/ Kukataa adhabu kwa makusudi. ix/Utoro na kushindwa kufanya mitihani ya ndani na ya nje. x/Kugoma, kuchochea na kuongaza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule, watu au jamii kwa ujumla. MAMBO MENGINE MHIMU

i/ Fomu ya kupima afya (medical examination) iliyojazwa na kusainiwa na Mganga wa Hospitali ya Serikali.

Ii/Tamko la mzazi la kukiri kukubali sheria na kanuni zilizotolewa na serikali au shule.

iii/ Maelezo binafsi ya historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika fujo na migomo.

iii/ Kila mwanafunzi aje na kivuli (copy) ya cheti cha kuzaliwa.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI RUSESA

.....

EMMANUEL P MAKOLE

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI RUSESA
S.L.P 354 -KASULU

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU

SHULE YA SEKONDARI RUSESA

FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

A. Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi

1. Jina kamili la mwanafunzi.....
2. Mahali anapoishi:

   Kijiji/mtaa..... Mkoa ..... wilaya .....

3. Tarehe ya kuzaliwa ..... Kijiji alichozaliwa .....

   kabila.....
4. Shule ya msingi aliyosomea.....

Habari za wazazi / walezi

1. Jina kamili la baba /mlezi.....
2. Jina kamili la mama / mlezi.....
3. Kazi ya baba / mlezi..... .....

   Kazi ya mama / mlezi.....
4. Je baba yupo hai? ndio/ hapana.
5. Je mama yupo hai? ndio /hapana.

Kukitokea dharura ndugu wengine wanaoweza kujulishwa ni.

1. Jina kamili ..... uhusiano uliopo.....namba ya simu.....
2. Jina kamili..... Uhusiano uliopo.....namba ya simu.....

Mimi ..... Nathibitisha kuwa taarifa hizo ni sahihi na za kweli

Jina kamili la mzazi / mlezi .....

Saini .... Simu.....

B: Mkataba wa kutoshiriki katika migomo , fujo na makosa ya jinai.

Mimi ..... niliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari **Rusesa** kidato cha kwanza(01) mwaka **2021.**

1. Naahidi kutii na kutekeleza masharti na maelekezo mbalimbali ya shule chini ya uongozi wa shule hii. Sitashiriki katika migomo, fujo na makosa yoyote ya jinai

2. Kama mwanafunzi naahidi kuwa mtiifu na mnyenyekevu mahali popote kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria za shule hii

3. Endapo nitakiuka kanuni,taratibu na sheria za shule hii **nastahili kuadhibiwa kulingana na itakavyoelekezwa na kuamliwa na mwalimu, mkuu wa shule na bodi ya shule kwa ajili ya kurekebisha mwenendo wangu,** kuleta heshima ya shule, kuleta amani na utulivu shuleni na kuendeleza malezi bora kwa vijana wa Tanzania.

4. Nathibitisha kuwa nimesoma kwa makini na matamko haya nayatoa kwa ajili yangu mwenyewe .

   Jina la mwanafunzi.....

   Saini ..... **tarehe** .....

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU
SHULE YA SEKONDARI RUSESA

Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

1. Mimi .....mzazi/mlezi wa mwanafunzi.....aliyechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Rusesa mwaka 2021.

2. Nakubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule kwani natambua kuwa malezi bora ya mtoto ni matunda kati ya walimu na wazazi/ walezi

3. Aidha natambua kuwa nidhamu ina mchango mkubwa katika maendeleo mazuri ya kitaaluma ya mwanafunzi

4. Hivyo nitakuwa tayari kusaidiana na walimu kutoa malezi bora kwa mwanafunzi huyu kuanzia nyumbani akiwa katika jamii na akiwa shuleni

5. Mwisho, nitakuwa tayari kupokea ushauri na maelekezo kutoka kwa walimu, uongozi wa shule na bodi ya shule kwa ajili ya kumlea mwanafunzi ili awe na mwenendo unaokubalika shuleni na katika jamii kwa ujumla .

Jina kamili la mzazi/mlezi.....

Namba ya simu.....

Saini..... **tarehe**.....

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
RUSESA SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by a medical officer in respect of all form one (I) entrance)

Student's full name .....

Age .....(years).....Sex.....

Stool examination.....

Urinalysis ..... Blood count (white and white) .....

.....

Syphilis test.....

.....

T.B Test .....

.....

Eye test.....

.....

Spleen.....

.....

Additional information e.g physical defect impairment(s), chronic infections or family disease

.....

.....

.....

.....

I certify that I have examined above student and recommended that he/ she fit /unfit to pursue further education .

Signed.....Designation.....Officialstamp.....Date.....

(Delete whichever is in applicable)